Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

# HALI YA USALAMA WA CHAKULA KWA TANZANIA BARA

## KULINGANA NA TAKWIMU ZA UTAFITI WA MAPATO NA MATUMIZI YA KAYA BINAFSI 2017-18


Septemba 2024

NATIONAL BUREAU OF STATISTICS
NBS
TANZANIA
STATISTICS FOR DEVELOPMENT

Tanzania Food and Nutrition Centre

# Dondoo Kuhusu Tanzania Bara

## Mgawanyo wa Idadi ya Watu kwa Mikoa




*Chanzo: Sensa ya Watu na Makazi Tanzania 2022*

# Dondoo Muhimu Kuhusu Tanzania Bara



| | |
|---|---|
| Idadi ya Watu | **59,851,347** |
| Mjini | **20,618,348** |
| Kijijini | **39,232,999** |



Wastani wa watu katika kaya **4.3**



| | |
|---|---|
| Wanaume | **29,137,638** |
| Mjini | **9,890,218** |
| Kijijini | **19,247,420** |



| | |
|---|---|
| Wanawake | **30,713,709** |
| Mjini | **10,728,130** |
| Kijijini | **19,985,579** |



- Mchango wa sekta ya kilimo katika Pato la Taifa ni asilimia **26.5.**
- Asilimia **63.4** ya kaya zinajishughulisha na kilimo.



- Asilimia **26.4** ya watu wa Tanzania Bara wana umaskini wa mahitaji ya msingi, wakati asilimia **8.0** ya watu wanaishi katika umaskini wa chakula.



- Uwiano wa kujitosheleza kwa mazao ya nafaka na yasiyo ya nafaka kwa Tanzania Bara kwa mwaka wa matumizi 2023/24 ni asilimia **124**.

*Chanzo: Sensa ya watu na makazi 2022; Utafiti wa Kilimo wa Mwaka 2022/23; Hali ya Uchumi wa Taifa katika mwaka 2023, HBS 2017/18 na Taarifa ya Tathimini ya Mwisho ya Uzalishaji wa Mazao ya Chakula kwa Msimu wa 2022/23 na Upatikanaji wa Chakula Nchini kwa Mwaka 2023/24, Wizara ya Kilimo*


# Dondoo Muhimu Kuhusu Tanzania Bara

## Aina za Utapiamlo Miongoni mwa Watoto Chini ya Umri wa Miaka Mitano



Ukondefu 3.3%

(Uzito mdogo ukilinganisha na kimo/urefu)



Udumavu 30.0%

(Kimo/Urefu mdogo ukilinganisha na umri)




Uzito Pungufu 12.1%

(Uzito mdogo ukilinganisha na umri)

## Uzito uliozidi/Unene kupita kiasi kati ya Umri wa Miaka 20 - 49

Wanaume 17.0%



Wanawake 36.0%

## Huduma ya Maji na Usafi wa Mazingira



Asilimia 72.8 ya kaya zinapata maji ya kunywa kutoka kwenye vyanzo vilivyoboreshwa.



Asilimia 74.4 ya kaya zinatumia vyoo vilivyoboreshwa.

*Chanzo: Utafiti wa Afya ya Uzazi na Mtoto na Viashiria vya Malaria wa Mwaka 2022 (TDHS-MIS)*

# Dondoo za Uchambuzi wa Matumizi ya Chakula Tanzania Bara kwa kuzingatia Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi Tanzania Bara 2017-18

## Wastani wa Kalori kwa Mtu kwa Siku kwa Eneo

| | |
|---|---|
| Tanzania Bara | 2,046 |
| Kijijini | 2,071 |
| Mjini[1] | 1,964 |
| Dar es Salaam | 2,058 |
| *Inayopendekezwa kwa Tanzania Bara[2]* | *2,300* |






## Wastani wa Kalori kwa Mtu kwa Siku kwa Watu Maskini na Wasio Maskini

| | |
|---|---|
| Watu Maskini | 2,046 |
| Watu wasio Maskini | 2,071 |
| *Inayopendekezwa kwa Tanzania Bara[2]* | *2,300* |

## Mgawanyo wa Kalori kwa Chanzo cha Upatikanaji na Eneo





*[1] Mjini inahusisha maeneo ya mjini nje ya Dar-es-Salaam*
*[2] Mwongozo wa Lishe Bora kwa ajili watu wenye afya Tanzania Bara*

**Vyakula Vilivyoliwa na Angalau Asilimia 30 ya Kaya katika Mwezi Uliopita Kulingana na Eneo**

| Chakula | Kijijini | Mjini | Dar es Salaam |
|---|---|---|---|
| Mchele wa Mbeya | 19.3 | 36.8 | 62.4 |
| Mchele wa Morogoro | 16.5 | 24.4 | 34.3 |
| Mkate wa slesi | 3.4 | 20.8 | 38.0 |
| Unga wa ngano | 31.9 | 53.6 | 58.1 |
| Chapati | 9.3 | 18.3 | 44.3 |
| Unga wa mahindi (sembe) | 97.6 | 99.1 | 99.9 |
| Nyama ya ng'ombe mchanganyiko | 38.8 | 64.1 | 65.0 |
| Samaki wabichi wa maji chumvi | 10.0 | 22.0 | 32.1 |
| Samaki wakavu | 31.6 | 35.8 | 16.1 |
| Dagaa wakavu | 63.4 | 64.7 | 52.6 |
| Samaki wabichi waliokaushwa | 15.9 | 20.0 | 39.1 |
| Mafuta ya alizeti au mbegu za alizeti | 54.4 | 63.6 | 49.6 |
| Ndizi za kupika | 20.2 | 31.7 | 31.0 |
| Nazi | 9.6 | 19.5 | 48.5 |
| Mchicha | 56.5 | 67.6 | 62.5 |
| Majani ya viazi | 25.5 | 35.8 | 50.6 |
| Majani ya maboga | 40.9 | 31.6 | 14.6 |
| Nyanya | 85.5 | 93.9 | 86.4 |
| Bamia | 22.2 | 24.7 | 37.7 |
| Pilipili hoho | 7.0 | 26.4 | 45.9 |
| Maharage ya soya | 16.5 | 21.4 | 57.3 |
| Maharage makavu | 67.5 | 71.8 | 34.9 |
| Vitunguu mviringo | 73.4 | 91.0 | 84.6 |
| Karoti | 6.4 | 25.4 | 54.2 |
| Viazi mviringo | 16.8 | 35.8 | 32.1 |
| Viazi vitamu | 35.6 | 35.9 | 14.7 |
| Sukari ya kahawia | 48.2 | 72.1 | 70.3 |
| Majani ya chai | 34.0 | 48.3 | 47.1 |
| Chakula (migahawani) | 16.1 | 27.3 | 42.6 |
| Chakula na vinywaji vinavyouzwa na mtembezaji wa mtaani | 13.7 | 18.5 | 46.8 |
| Chakula (kantini) | 15.2 | 24.7 | 41.7 |
| Vinywaji baridi (kantini) | 9.1 | 14.6 | 31.8 |


*[1] Vyakula vilivyoliwa na angalau asilimia 30 ya kaya kijijini, mjini au Dar es Salaam vimejumulishwa kwenye orodha*

## Ulaji wa Matunda na Mbogamboga kwa Mtu kwa Siku kwa Eneo





*WHO wanapendekeza kwa siku gramu 400 za matunda na mbogamboga kwa mtu*

## Wastani wa Gharama za Kalori 1,000 kwa Kaya kwa Eneo








## Mgawanyo wa Matumizi ya Chakula kutoka kwenye Jumla ya Matumizi yote kwa Eneo



# Mgawanyo wa Kalori kwa Makundi ya Vyakula



## Mlinganisho wa Kalori kutoka Makundi ya Vyakula na Mwongozo wa Chakula na Ulaji Tanzania Bara




**Watu wa Tanzania Bara wanatumia:**

- Zaidi kuliko inavyopendekezwa vyakula vya nafaka, mizizi yenye wanga na ndizi za kupikwa.
- Chini ya kiwango kuliko inavyopendekezwa matunda, mbogamboga, vyakula vyenye asili ya wanyama; vyakula jamii ya kunde, karanga na mbegu zenye mafuta; na mafuta ambayo ni salama kwa afya.

*Angalizo: Mwongozo wa Chakula na Ulaji unapendekeza kupunguza matumizi ya sukari.*

# Mlo Kamili



*Asilimia 31.4 ya watu Tanzania Bara wanakula mlo kamili.*

| Asilimia ya Watu Wanaokula Mlo Kamili kwa Eneo | |
|---|---|
| Kijijini | 22.7 |
| Mjini | 44.6 |
| Dar es Salaam | 62.6 |


| Asilimia ya Watu Maskini na Wasio Maskini Wanaokula Mlo Kamili | |
|---|---|
| Watu Maskini | 16.6 |
| Watu Wasio Maskini | 36.8 |


**Mgawanyo kwa Asilimia wa Virutubishi Vikuu katika Mlo Kamili kwa Watu Maskini na Wasio Maskini**

| | Mafuta | Wanga | Protini |
|---|---|---|---|
| Tanzania Bara | 15.7 | 68.9 | 12.3 |
| Watu Maskini | 11.8 | 72.7 | 12.1 |
| Watu Wasio Maskini | 15.7 | 68.9 | 12.3 |

*Kulingana na WHO/FAO (2003), Mlo kamili unapaswa kujumuisha 10-15% ya Protini, 15-30 % ya Mafuta na 55-75% Wanga.*

Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi Tanzania Bara (HBS 2017/18), ulitekelezwa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) kwa kushirikiana na Idara ya Kuondoa Umaskini ya Wizara ya Fedha na Mipango (MoFP). Utafiti huu ulipata Fedha kutoka Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Wadau wa Maendeleo ambao ni pamoja na Benki ya Dunia (WB), Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Masuala ya Wanawake (UN Women), Ubalozi wa Ireland, Ubalozi wa Sweden, Shirika la Umoja wa Mataifa la linaloshughulikia Watoto (UNICEF) na Shirika la Msaada la Canada (GAC). Msaada wa kitaalam ulitolewa na WB, UN Women na UNICEF.




Mwongozo wa Chakula na Ulaji Tanzania Bara (TFBDG) ni mwongozo wenye msingi wa ushahidi juu ya tabia bora ya ulaji na mitindo ya maisha inayolenga kutoa msingi wa chakula na lishe kwa umma, sera za afya na kilimo, na programu za elimu ya lishe. Wanatoa ushauri juu ya vyakula, makundi vya chakula na mifumo ya lishe ili kutoa virutubisho muhimu kwa afya na kuzuia magonjwa yanayohusiana na lishe. Marejeo: Wizara ya Afya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. 2023. *Mwongozo wa Chakula na Ulaji*. *Tanzania Bara*. *Ushauri wa Kitaalam*. Wizara ya Afya: Dodoma, Tanzania.

Uchambuzi katika taarifa hii umetayarishwa mwaka wa 2023/24 kwa msaada wa kiutaalam kutoka COMESA na Ofisi ya Takwimu Norway chini ya mradi wa "Takwimu za Usalama wa Chakula" unaofadhiliwa na Shirika la Ushirikiano wa Maendeleo la Norway (Norad).